**Learning by Ear 2010**

**Theme: Illiteracy and education**

**“A GIRL FINISHING SCHOOL”**

**Episode 07:** "Njia ya mkato:Haina manukato’’

**Author:** Frédéric GAKPARA

**Editor:** Yann Durand

**Translator:** Anne Thomas

**Characters:**

**Latifa** *(Ana umri wa miaka 18, ni binti yao Papa Wali na Mamoua. Anasoma mwaka wa tatu wa masomo yake ya daktari msaidizi. Ni mwerevu wala hajawahi kurudia darasa lolote. Amekuwa akiishi mjini pamoja na kaka yake kwa muda wa miaka miwili.)*

**Elinam** *(Ana umri wa miaka 22. Ni mwanao Papa Wali na Mamoua. Kakake Latifa. Anasoma mwaka wa nne katika chuokikuu jijini kilomita kiasi 120 kutoka nyumbani kwa wazazi wake katika mji mdogo.)*

**Zakia** *(Mwanamke mwenye umri wa miaka 23, ni mwanamke mwenye uhuru wa kujitendea mambo, ni rafiki wa dhati wa Latifa na amepandishwa cheo kuwa mkurugenzi wa utangazaji wa shirika lake la Safari za Kitalii na angali akifanya kazi katika mji mdogo ambao yeye na Latifa wanatoka.)*

**The visitor** *(Mwanamume mwenye asili ya Kieshia na ana umri wa miaka 40)*

**INTRO**

**Hujambo msikilizaji na karibuni kwenye sehemu ya saba ya''Mtoto wa kike ahitimu shuleni" katika kipindi cha Noa Bongo-Jenga Maisha yako.Kipindi hiki kinaelezea masuala ya elimu na kutojua kusoma na kuandika.**

*Alipowasili jijini, Latifa hakuchukua muda mrefu kuzizoea harakati zake. Nafasi ndogo katika chumba cha kakake, gharama ya maisha, kelele, mazingira machafu ..yote hayo yalikuwa mambo magumu ila hakuwa na na njia nyengine itakayomfikisha kwenye lengo lake. Alihudhuria madarasa yake yote katika Chuo cha Madaktari Wasaidizi na akajitahidi kujibana kimaisha kwa kuwa hakutaka kumtatiza kakake.*

*Kadri miaka ilivyopita ndivyo hali ilivyozidi kuwa ngumu na akalazimika kujibana zaidi.Msichana huyo wa umri wa miaka 18 sasa anasoma mwaka wake wa mwisho na urembo wake umeanza kuwazuzua watu. Usiku wa leo, Latifa anakabiliana na kaka yake.Sikiliza sehemu ya saba iitwayo:* ***"Njia ya mkato:Haina manukato"***

**Scene 1, IN ELINAM'S ROOM**

Latifa na Elinam

1. **SFX ATMO: HOME SOUNDS IN THE CITY. SOUND OF FOOTSTEPS IN THE CORRIDOR. PEOPLE COOKING. SOUNDS OF POTS AND PANS. RADIO CAN BE HEARD FROM ONE ROOM, MUSIC FROM ANOTHER. TRAFFIC FROM THE DISTANCE.**

2. **Elinam:** (**Very angrily**) Nakuuliza mara ya mwisho, Latifa. Hii simu ya mkono umeipata wapi?

3. **Latifa:** Nimepawa na rafiki yangu.

4. **Elinam:** Jina lake nani? Anafanya kazi gani?

5. **Latifa:** Serge. Anauza magari.

6. **Elinam:** Kwanini amekupa simu ya mkono? Mna uhusiano gani na yeye?

7. **Latifa:** Alitaka tuwe na uhusiano wa ziada lakini sikuridhia.

8. **Elinam:** Ulikataa mambo ya mapenzi kisha akakupa simu ya mkononi?Jee ungekubali angekupa nini ? Gari?

9. **Latifa:** (**Silence**) …

10. **Elinam:** Ndiye aliyekupa hizo fedha zilizokuwa kwenye mkoba wako?

11. **Latifa:** Elinam! **(stuttering)** Vipi, mbona…!! Hapana!

12. **Elinam:** Nani aliyekupa basi?

13. **Latifa:** (**Silence**) Patrick.

14.**Elinam:** Alaa! Na pengine anafanya kazi ya benki?

15.**Latifa:** (**Silence**) Anafanya kazi katika shirika la bima.

16.**Elinam:** Kwani ni mpenzi wako?

17.**Latifa:** Hajawahi kutaka tuwe wapenzi. Amejitolea tu kunipeleka chuoni na kunirejesha nyumbani usiku.

18.**Elinam:** Latifa, sikudhani kwamba bado hujakomaa kiakili. Hawa ni wanaume waliooa na familia zao. Kazi yao ni kuzitelekeza familia zao na kukimbizana na visichana vidogo!

19.**Latifa:** Wewe una simu ya mkononi,sivyo ? Katika chuo chenu kuna basi la kuwapeleka. Unajua chuo changu kiko wapi? Kwani ni hatia kwa mtu kujitolea kunipeleka kwa gari lake?

20.**Elinam:** Ni hatia kuwekwa unyumba na wanaume ambao wameoa! Hasa tukizingatia kuwa msichana anayehusika ana umri wa miaka 18 tu!

21.**Latifa:** Wao ndio wanaoniandama! Sijamuomba mtu yeyote chochote!

22.**Elinam:** Inakubidi ujifunze namna ya kuvikataa baadhi ya vitu unavyopawa! Baba ndiye aliyenipa simu yangu ya mkono! Nilijitahidi sana hadi nikapata ufadhili wa masomo yangu. Aidha kila jioni ninafanya kazi ya kusomesha ili tupate fedha za kula na kugharamia mambo mengine tunayohitaji. Sina mwanamke mzee anayeyafadhili mahitaji yangu!

23.**Latifa:** (**Silence**) …

24.**Elinam:** Sharti uirejeshe simu ya watu! Umenielewa?

25.**SFX ATMO** **DOOR SLAMS LOUDLY**

**<u>Scene 2, IN ELINAM'S ROOM</u>**

Latifa na Zakia on the telephone.

26.**SFX ATMO:** **RUMMAGING IN A BAG.**

27.**SFX ATMO:** **DIALLING OF A NUMBER ON A MOBILE TELEPHONE**

28.**Zakia:** Hallo?

29.**Latifa:** Hallo! Mambo vipi Zak! Latifa hapa!

30.**Zakia:** Latifa! Muda mrefu hatujawasiliana!Kila nikimpigia kakako simu sikupati.Wakati mwingine hupiga simu usiku sana ila hupo. Kwani kuna nini?

31.**Latifa:** Nimechoshwa na hali hapa nyumbani. Tumegombana tena!

32.**Zakia:** Kwanini?

33.**Latifa:** Kwasababu ya simu hii ninayokupigia kwayo.

34.**Zakia:** Kwani ni simu ya nani?

35.**Latifa:** Rafiki yangu alinipa na Elinam ameniamba nimrejeshee mwenyewe. Huoni kama amezidi?

36.**Zakia:** Inategemea ni rafiki wa aina gani na kilichomfanya yeye kukupa hiyo simu!

37.**Latifa:** Anaitwa Serge. Alitaka tuwe na uhusiano wa kimapenzi nikakataa. Kisha akanipa simu ya mkono.

38.**Zakia:** Kwa hivyo alitaka kukuhonga? Hatari hiyo, Latifa!

39.**Latifa:** Sina nia ya kuwana uhusiano wa kimapenzi na mtu ambaye ni mzee kama babangu!

40.**Zakia:** Basi usijiingize kwenye mtego!

41.**Latifa:** Kwa hivyo unadhani ni vyema nikirejesha simu?

42.**Zakia:** Nini ulichomtendea rafiki yako hata akupe simu?

43.**Latifa:** Wala!Hakuna nlichokifanya!

44.**Zakia:** Basi, mrejeshee mwenyewe, Latifa! Unakumbuka tulivyokuwa tukisema? Kwamba wanaume wana dhana kwamba wanawake ni wavivu na wanapenda kuwategemea wanaume?

45.**Latifa:** Ndiyo, nakumbuka.

46.**Zakia:** Waonyeshe kwamba wewe si mwanamke sampuli hiyo- mwanamke si lazima amtegemee mwanamume!

47.**Latifa:** Zak, mwanamume akijitolea kunipeleka chuoni asubuhi na kunirejesha nyumbani jioni kwa gari lake, hiyo si hisani?

48.**Zakia:** Anatenda hilo pia?

49.**Latifa:** Hapana, si yeye! Ninamzungumzia Patrick.

50.**Zakia:** Ndiye nani huyo? Mpenzi wako?

51.**Latifa:** Hapana! Hajasema lolote mpaka sasa! Kuna mara alinipa fedha za kujinunulia nguo mpya.

52.**Zakia:** Ana umri gani?

53.**Latifa:** Pengine 40 au 45 …sina uhakika

54.**Zakia:** Latifa! Labda ameoa! Hawa mabwana hawafanyi mambo hayo bure. Usijitafutie balaa kwa hisani yako!

55.**Latifa:** Kwa hivyo nisikubali anipeleke chuoni, sawa?

56.**Zakia:** Ni suala la maadili, Latifa! Baada ya muda usio mrefu utafuzu na utapata kazi nzuri. Usishiriki mambo ya watu wasije kudai hisani walizokutendea. Zaidi ya hayo, wenzako watakuchukulia vipi wakiona unasindikizwa na mtu ambaye hamna uhusiano wa kinasaba?

57.**Latifa:** Sawa, Zak… Ninakuahidi nitajirekebisha! Lakini niamini nikwambiayo. Nimekataa katakata habari ya kuwa na uhusiano wa kimapenzi na mtu!

58.**Zakia:** Natumai hivyo, Latifa. Vipi hali kwa jumla?

59.**Latifa:** Nina upweke kidogo. Sina marafiki wa dhati hapa. Ninatamani sana mwaka huu uishe. Ninakumbuka sana Zak! Vipi hali yako kimaisha?

60.**Zakia:** Mambo yananiendea vyema! Nimepandishwa cheo na kuwa mkurugenzi wa utangazaji wa kampuni yetu ya kitalii kiasi miezi minne iliyopita!

61.**Latifa:** Raha iliyoje! Basi, wewe ni mkubwa kazini kwako?

62.**Zakia:** Unaweza kusema hivyo. Tutaonana kiasi miezi mitatu ijayo kwasababu tutakuwa na kibanda kwenye maoyesho ya kibiashara yatakayofanyika huko jijini.

63.**Latifa:** Kweli? Mambo mazuri hayo!

64.**Zakia:** Tutakuwa na kiasi wiki mbili kujikumbusha tulikotoka!

65.**Latifa:** Nina hamu kuu ya kukukona Zak!

66.**Zakia:** Haya, tutaonana baada ya muda si mrefu basi.

67.**Latifa:** Sawa! Asante sana kwa ushauri wako!

**MUSIC**

68.**NARRATOR:** *Marafiki hao wawili walitamani sana siku ya maonyesho ya kibiashara ifike. Kampuni ya kina Zakia ilipangiwa kushiriki kwenye maonyesho hayo. Marafiki hao walipanga kukutana siku ya ufunguzi wa maonyesho hayo. Hatimaye siku iliwadia. Latifa ameandamana na kaka yake Elinam. Anamwona Zakia ambaye sasa amebadilika kwa kiasi kikubwa. Mwanamke huyo anapendeza kwa urembo wake hapo alipo kwenye kibanda chao.*

## Scene 3, AT THE FAIR

Elinam, Latifa, Zakia na mgeni

69.**SFX ATMO: TRADE FAIR HALL, SOUND OF STEPS (ONE MAN&ONE WOMAN WALKING), DISCUSSIONS, DIFFERENT MUSIC**

70.**Zakia:** (**Shouting from the distance**) Hapa! Latifa njoo huku!

71.**Latifa:** (**Very enthusiastically)** Ewe!, Elinam, Tizama kule, Zakia yule pale!

72.**Elinam:** (**Surprised**) Kweli?

73.**Zakia:** (**Shouting from the distance**) Njooni kwenye kibanda changu! Fuateni uchochoro huo mwengine, ni rahisi kidogo kufikia niliko!

74.**Latifa:** (**Shouting**) Sawa, twaja!

75.**Elinam:** (**In shock**)Yule ni Zakia kweli? Haiwezekani!

76.**Latifa:** Bila shaka ndiye! **(teasing him)** ahaa, una maana kwamba amekuwa mrembo zaidi kuliko hapo awali?

77.**Elinam:** (**Trying to get a grip of himself**) Aha! Urembo hauna viwango!

78.**Latifa:** **(teasing him)** Usione haya! Kubali kwamba amekuvutia!

79.**Elinam:** (**In a low voice**) Yaishe nawe!

80.**SFX:** **FOOTSTEPS**

81.**Zakia:** Latifa, Elinam! Nimefurahi sana kuwaona!

**THEY KISS EACH OTHER ON THE CHEEK.**

82.**Latifa:** Na mimi pia nimefurahi kukuona tena, Zakia! Nusra tupotee. Maonyeshe haya ni makubwa sana!

83.**Zakia:** Ndiyo, bado sijapajua vizuri. Latifa umenawiri! Umekuwa mwanamke sasa! Singekutambua lau msingekuwa pamoja na Elinam!

84.**Latifa:** Na wewe je! Ulivyo unapendeza si haba! Utadhani umeshakuwa mkurugenzi mtendaji!

85.**Zakia:** **(laughing)** Umezidi nawe! Jitazame! Umekomaa kiasi cha kuzua rabsha... sasa ninafahamu! Kaeni kidogo! Samahani Elinam, hatujaonana kwa miaka zaidi ya miwili....

86.**Elinam:** Lakini hujaniona kwa miaka zaidi ya minne!

87.**Zakia:** Usione wivu! Nimekutambua mara moja. Hujabadilika sana! Sema hizo ndevu tu....Unafanya kipi maishani?

88.**Elinam:** Uhandisi. Ninatarajia kuhitimu kiasi miezi miwili ijayo. Kitambo sana hatujafika nyumbani... mamako hajambo?

89.**Zakia:** Ndiyo, hana neno! Aghalabu hupitia kwenye karakana ya babako. Alinipa gunia la mchele niwaletee. Anaonekana mchovu kila kukicha.

90.**Elinam:** Kweli? Na mama je?

91.**Zakia:** Aliniambia kuwa mamako hajambo. Sidhani kwamba mambo baina yao yametengemaa tangu Latifa alipoondoka... Souleyman naye ameshika urafiki na watu wenye tabia zisizoeleweka. Hata shule haendi tena.... Anavuta sigara.

92.**Elinam:** **(shocked)** Unasema nini? Na umri wake huo wa miaka 14?

93.**Zakia:** Babako hamtaki nyumbani kwake tena. Kila mara huwa kuna ugomvi na Mamoua anamtetea.

94.**Latifa:** Wala sishangai! Umezungumza na Souleyman?

95.**Zakia:** Unajua vyema siwezi kwenda nyumbani kwenu. Epiphane ndiye huniarifu mambo ya jamaa zenu kila ninapopitia kwenye karakana ya babako.

96.**Latifa:** Aaaha, Kweli? Yeye hajambo?

97.**Zakia:** Anaelekea kuwa msimamizi sasa hivi! Ndiye anayesimamia kila kitu katika karakana hiyo. Alipita kwenye madarasa yake yote na hivi sasa amejisajili kupata mafunzo ya ziada ya ufuaji vyuma... huyo bwana atakuja fanikiwa sana siku za usoni!

98.**Elinam:** Hivyo basi biashara inazidi kuimarika?

99.**Zakia:** Ndiyo kwa kweli. Epiphanie ni mbunifu. Anatengeza sampuli mpya za bidhaa na pia hutoa kandarasi kwa kazi ambazo hawana mashine zinazofaa kwenye karakana yao. Nimemhimiza achapishe vikaratasi vya maelezo mahsusi kwa wageni wanaozuru karakana yao,na pia anapeleka matangazo kwenye vituo vya redio.

100. **SFX:** **FOOTSTEPS APPROACHING**

101. **The visitor:** Habari za jioni! Ninaomba kuzuru kibanda chenu hiki!

102. **Zakia:** Karibu kwenye kibanda cha kampuni yetu iitwayo Trails of Africa Agency. Mimi ndiye nitakayekuongoza!

103. **The visitor:** Asante!

104. **Zakia:** (**In a low voice to Elinam and Latifa**) Tembeleeni vibanda vinginevyo kisha tutakutana baadaye...

105. **Elinam:** Sawa!

106. **Latifa:** Baadaye!

107. **Zakia:** (**To the visitor**) Kampuni yetu inaandaa ziara za siku 15,ambapo utayatembelea maeneo kadhaa ya kihistoria,sehemu zenye mandhari ya kuvutia, masoko sita tofauti ya bidhaa za usani, fursa ya kutumbuizwa na ngoma za kiasili na za kidini...**(fade out)**

## MUSIC

**OUTRO**

*Ingawa ana kazi nyingi, Zakia anafanikiwa kuwaona Latifa na kakake Elinam mara kadhaa wakati maonyesho ya kibiashara yakiendelea. Latifa na Elinam wanawanunulia zawadi jamaa zao walioko nyumbani akiwemo Epiphane. Hata hivyo Elinam anajuta kwani hakumwambia Zakia hisia zake kwake. Anadhani huenda ikawa vigumu kumpata Zakia kwa jinsi alivyojiimarisha kikazi. Jee ni kweli kwamba mapenzi ndiyo mambo yote? Vipi hisia za Zakia? Na vipi hali ya Latifa kuhusiana na mambo haya?Atapata mahali pa kukaa?*

*Ili kufahamu zaidi, sikiliza sehemu itakayofuata ya "Mtoto wa kike* ahitimu *shule", katika makala inayohusu elimu na kutojua kusoma na kuandika.*

**Ukitaka kukisikiliza kipindi hiki au vipindi vyengine vyote vya Noa Bongo-Jenga Maisha yako, tizama ukurasa wetu wa wavuti www.dw-world.de/lbe. Unaweza pia kutuandikia barua-pepe.Anwani ni :** lbe@dw-world.de.Na mpaka hapo ndipo tunapokomea kwa leo.

**Shukran sana kwa kujiunga nasi hadi wakati mwengine,kwaheri!**

**END OF 7th EPISODE**